# NI KANISA MOJA TU!

Kristo alisema; ***"…nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu*** *{yaani, nguvu za giza}* ***haitalishinda" Mathayo 16:18.*** Baada ya hapo, aliendelea mbele zaidi na kuanza kulijenga. Ni nini hasa alichojenga? *{Kwa maelezo zaidi, agiza ujumbe wetu usemao* ***"KANISA NI NINI?",*** *ili ujifunze zaidi, na tutakutumia bure ujumbe huo}.* Kristo alikuja akitangaza *{akihubiri}* habari fulani ihusuyo ujio wa ufalme wa Mungu hapa duniani pamoja na maisha ya ufalme huo *{yaani, haki yake}.* Tunafahamu kwamba mwanadamu aliumbwa ili aishi hayo maisha ya kimungu, lakini alidanganyika na kwenda kando ya maisha hayo. Kristo alipokuwa akiendelea kutangaza habari hizi, watu waliziamini na kumfuata. Ni nini walichokiamini? Waliyaamini maisha ambayo Kristo aliyafundisha. Walikubali kwamba hayo ndiyo maisha ya kweli wanayopaswa kuyaishi. Basi ni hao walioamini ndio aliowapa jina la Kanisa, ama kuwaita kuwa ni Kanisa lake. Eleweni hapa tafadhalini kwamba; si watu wanaokaa chini na kuamua kuanzisha ushirika. Si mtu anayepiga kampeni na kuwashawishi watu wengine kukubaliana naye, na kutengeneza kundi ambalo litafanya yale tu ayasemayo. Walikuwa *{na mpaka sasa}* ni watu waliolisikia neno la Mungu lililohubiriwa na Yesu, na baadaye kupitia kwa watu aliowafundisha ujumbe ule ule, naam; watu ambao walipolisikia neno la Mungu likihubiriwa, ***"…walilipokea si kama neno la wanadamu, bali kama neno la Mungu; na ndivyo lilivyo kweli kweli; litendalo kazi pia ndani yenu ninyi mnaoamini" 1 Wathesalonike 2:13.*** Kwa hivyo kwamba ni kwa Yesu, ama Manabii, ama Mitume, kile waaminio walichokikubali ni mfumo mmoja wa maisha ya Mungu uliohubiriwa na wote, na ambao uliandikwa na kuwa Maandiko Matakatifu tunayoyanukuu hapa.

Kwa hivyo hapa tunamzungumzia Mungu mmoja, mwenye njia *{mfumo/aina}* moja ya maisha, ambayo wale watu wanaoitwa Kanisa waliikubali na wanajifunza kuishi kwayo. Kwa hivyo basi, ni ukweli ulio wazi kwamba; kadiri watu wengi wanavyoendelea kuyakubali maisha haya, ndivyo pia wote wanavyounganishwa katika ***"nia moja na shauri moja", soma 1 Wakorintho 1:10.***

Sasa basi; inawezekanaje watu wengi kuwa na nia moja? Ni rahisi sana! Baada ya kuukubali mfumo mmoja wa maisha ya Mungu ulio katika Kristo Yesu; basi hawaishi ***"tena kwa ajili ya nafsi zao wenyewe*** *{si kulingana na fikira na matakwa ya mtu},* ***bali kwa ajili yake yeye aliyekufa akafufuka kwa ajili yao" 2 Wakorintho 5:15.*** Kwa hivyo, wajapokuwa wengi, kila mmoja anasahau *{anatupilia mbali}* nia yake ya awali na kuchukua ***"nia ya Kristo",*** ambayo pia ndiyo nia ya Mungu ***{soma 1 Wakorintho 2:16; Yohana 17:21}.***

# KWANINI UMOJA?

Wakati Mungu alipomuumba mwanadamu, alikusudia kuipanua/kuiongeza familia yake yenye kuishi maisha yake yaliyo makamilifu na matakatifu. Baada ya mwanadamu kuchagua maisha mabaya, alijiletea ufahamu ambao mtu anapoutumia, unasababisha migawanyiko yote hii tuionayo katika jamii leo *{Kwa msaada zaidi, agiza ujumbe wetu usemao **"HUYU NI SHETANI"**, ili ujifunze zaidi, na tutakutumia bure ujumbe huo}.* Kwa kuwa ni lazima aukamilishe mpango wake, basi Mungu alimtuma Yesu aliyekuja na kuufunua *{kuuweka wazi}* ufahamu wa kweli ambao ukitumiwa, utawaunganisha wote katika familia ya Mungu aliyokusudia kuifanya. Kanisa ni wale waliyoyakubali haya maisha, na Mungu amewafanya kuwa Mabalozi *{wawakilishi}* wake hapa duniani katikati ya wanadamu waliogawanyikana wao kwa wao. Ni kwa kusudi gani? Naam; ni kwa kusudi la ***"…kuwaangaza watu wote wajue habari za madaraka ya siri hiyo, ambayo tangu zamani zote ilisitirika katika Mungu aliyeviumba vitu vyote; ili sasa, kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane…" Waefeso 3:9-10.***

Kwa hivyo Kanisa halitakuwa Kanisa, na wala halitamtumikia Mungu ikiwa halioneshi ile nia moja ya Kristo ambayo kwayo Mungu huliunganisha pamoja na kuwa ***"…kama vile mwili ni mmoja, nao una viungo vingi, na viungo vyote vya mwili ule, navyo ni vingi, ni mwili mmoja; vivyo hivyo na Kristo*** *{yaani, Kanisa}**" 1 Wakorintho 12:12,*** soma pia ***Waefeso 4:15.*** Kanisa likiungana katika namna hii, basi litaushawishi ulimwengu kwamba linamwakilisha Mungu na maisha yake ya kweli yaliyokusudiwa kwa ajili ya wanadamu wote bila kujali dini, jinsia, kabila, taifa, ukanda wala lugha; maana mwenye kanisa *{yaani, Yesu Kristo}* anasema kwamba; ***"wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako, hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma" Yohana 17:21.*** Tafadhalini fahamuni jambo hili kwamba; ni umoja ndio utakaouthibitishia ulimwengu kwamba watu hawa ni Kanisa la Mungu. Kinyume na ulimwengu wa Kishetani uliogawanyikana wenyewe, na kujawa na chuki; Mungu aliuweka ubalozi wake *{yaani, Kanisa lake}* ili kuufundisha ulimwengu njia ya amani, na kuionesha njia hiyo kwa namna hii ya umoja katika upendo kama uthibitisho; maana Kristo anazidi kusema kwamba; ***"Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi" Yohana 13:35.***

Wapendwa; jambo hili litawezekana pindi tu ambapo kila mshikika anajibidiisha katika kutaka kufanywa kuwa kama Mungu na kuacha kujishughulisha na mambo ya wengine ya kutaka kujua wanafanya nini, wanafikiri nini, wanasemaje, wanapenda nini n.k. Ni watu wasiofanya jambo lo lote kwa mawazo na matakwa yao wenyewe; bali katika mambo yote kuangalia kufanya sawa sawa na neno la Mungu ***{soma Mithali 3:5-6}.*** Basi mambo yakienda kwa njia hiyo; hakutakuwa na mtu adaiye kuwa ndiye mwenye kufanya jambo, wala atakaye kutumikiwa, wala aagizaye, wala lo lote la kimwili *{u-mimi/ubinafsi};* maana lo lote lifanyikalo ndani yao, wanamfahamu yule alifanyaye *{yaani, Kristo}*. Kama watu waliotumwa na Kristo na

kupewa uwezo wa kupanda, ama kupalilia, ama kukatia; naam, kwa lo lote lile alilopewa mtu kufanya, wanafahamu vyema kabisa kwamba ***"…apandaye si kitu, wala atiaye maji, bali Mungu akuzaye. Basi yeye apandaye, na yeye atiaye maji ni wamoja…" 1 Wakorintho 3:7-8.*** Wakiwa kama mradi wa Mungu, washirika hawa wa Kanisa hawana jambo lo lote lile la kugombania baina yao, maana kazi yao *{kupitia kwa karama za Mungu alizowapa kila mmoja wao}* ni kukua katika ufahamu wa Mungu, kwa kumtazama yeye *{na si mwanadamu}* katika kuthibitisha jambo na kutenda haki. Wanajifahamu wenyewe kuwa wao ni kazi ya Mungu, na hivyo wanamwachia yeye kila kitu katika kulinda na kutunza; kazi yao ni moja tu ya kuhakikisha kuwa wanafanya yale aliyoagiza Mungu *{na si wayatakayo wenyewe wala yatakayoletwa na mwingine}.*

## WAFUASI WA MUNGU

Mungu ni familia ambayo hivi sasa ina nafsi mbili ndani yake; yaani, Mungu Baba na Mungu Mwana ambaye awali alikuwa Neno ***{soma Yohana 1:1-3,14}.*** Hawa wawili wameunganishwa katika nia moja na shauri moja, maana Kristo anasema, ***"Mwana hawezi kutenda neno mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda; kwa maana yote ayatendayo yeye, ndiyo ayatendayo Mwana vile vile" Yohana 5:19.*** Kwa kuishi kwa mfumo mmoja wa maisha kunawafanya kuwa mmoja, maana Kristo anazidi kusema kwamba; ***"…mpate kujua na kufahamu ya kuwa Baba yu ndani yangu, nami ni ndani ya Baba" Yohana 10:38.*** Basi Mungu aliwaumba wanadamu ili kuiongeza familia yake na ***"kuwaleta wana wengi waufikilie utukufu {Waebrania 2:10}"*** na kwamba Kristo ***"…awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi" Warumi 8:29.*** Kwa kuwa mwanadamu alidanganyika; basi Mungu akalianzisha Kanisa lake ili kwa njia hiyo awafundishe wanadamu makusudi halisi ya maisha yao; na ili Kanisa lifanye hivyo, alilijenga katika msingi huu wa umoja wa Baba na Mwana, maana anasema; ***"…ushirika wetu ni pamoja na Baba, na pamoja na Mwana wake Yesu Kristo" 1 Yohana 1:3.*** Jambo hili lilikuwa dhahiri katika Kanisa la karne ya kwanza la Mitume na hata muda mrefu baada yao. Sikia kile kilichosemwa kuhusiana nao; kwamba ***"Na jamii ya watu walioamini walikuwa na moyo mmoja na roho moja; wala hapana mmoja aliyesema ya kuwa kitu cho chote alichonacho ni mali yake mwenyewe; bali walikuwa na vitu vyote shirika" Matendo 4:32.*** Tangia walipojifunza kwa Mungu, waliendelea kwa kufuata mfano huo huo wa Bwana wao; maana aliwaambia; ***"…nimewapa kielelezo; ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo" Yohana 13:15.*** Kanisa la mwanzo halikupoteza madhumuni ya kuanzishwa kwake ambayo ni kukua katika maisha ya kweli ya Mungu kama walivyoushuhudia ulimwengu kwa kusalia kuwa wamoja.

Hebu tupate uthibitisho zaidi tafadhalini. Baada ya Kanisa kukua na kutawanywa kwa mateso *{si kwa kudanganywa na kuiacha kweli},* po pote pale alipokuwepo mmoja au kadhaa, waliendelea kuhubiri kama walivyoonesha kwa mwenendo wa maisha yao. Je! walibaguana wao kwa wao kwa kila mmoja kuanzisha kundi lake, na kujidai kuwa mwanzilishi na kiongozi wake?

Tafadhalini tupate jibu kutoka katika Biblia. ***"Lakini wale waliotawanyika wakaenda huko na huko wakilihubiri neno*** *{maisha ya Mungu}.* ***Filipo akatelemka akaingia mji wa Samaria, akawahubiri Kristo. Na makutano kwa nia moja wakasikiliza maneno yale yaliyosemwa na Filipo…Na mitume waliokuwako Yerusalemu, waliposikia ya kwamba Samaria imelikubali neno la Mungu, wakawapelekea Petro na Yohana…", soma Matendo 8:4-7,14-16.***

Wapendwa; hebu na tuzungumzeni ukweli tafadhalini. Filipo alikwenda peke yake akihubiri na Wasamaria wakaamini. Je! alisema kwamba yeye ndiye mwanzilishi wa kundi hilo na hivyo kwamba lazima awe yeye kiongozi? Je! aliwaambia wenzake kwamba, *"ninyi hubirini huko na mimi nihubiri hapa, maana hawa ni wafuasi wangu; cha msingi tu ni kwamba sote tunamhubiri Kristo?"* Wapendwa; je! Filipo alifanya hivyo? La, hasha! Ni kwa nini basi yeye hakufanya hivyo? Ni kwa sababu lile alilolihubiri halikuwa neno lake. Kwa hivyo watu hawakumpokea yeye, bali walimpokea Mungu aliyemtuma. Kamwe hakujaribu kuwashawishi ili wakubaliane na matakwa yake. Alichofanya ni kuwaambia tu kuhusu maisha ya Mungu aliyogundua uzuri wake, na kwamba anatamani wao pia wayagundue na kupata amani kama yeye alivyopata.

Kadhalika Mitume waliokuwa Yerusalemu pia hawakusema kwamba, *"Sisi hatukumtuma Filipo, na hivyo mahubiri yake si halali, ni batili"*. Walifahamu kwamba, hakuna mtu awezaye kuongea ukweli isipokuwa tu kama ametumwa na Mungu, na kwamba pia hakuna awezaye kulithibitisha neno kwa ishara na miujiza isipokuwa Mungu aliyempa neno lake. Walichokifanya mara moja ni kutuma watu huko Samaria ili kuiimarisha kazi ya Mungu kwa kufanya sehemu yao baada ya kuwa Filipo amefanya sehemu yake; maana, ***"kila mmoja kwa kadiri alivyoipokea karama, itumieni kwa kuhudumiana; kama mawakili wema wa neema mbali mbali za Mungu. Mtu akisema, na aseme kama mahusia ya Mungu; mtu akihudumu, na ahudumu kwa nguvu anazojaliwa na Mungu; ili Mungu atukuzwe katika mambo yote kwa Yesu Kristo. Utukufu na uweza una yeye hata milele na milele. Amina" 1 Petro 4:10-11.***

Sasa je! baada ya Filipo, Petro na Yohana, kila mmoja kufanya sehemu yake *{na ni Mungu aliyefanya ndani yao},* kundi hilo lilikuwa la nani? Je! Kanisa la Samaria lilikuwa la Filipo? Ama je! lilikuwa la Petro na Yohana, kwa sababu kupitia kwao Mungu alilipatia roho wake mtakatifu? Katika historia yote ya Kanisa, tunaona Mungu akiongeza watu katika Kanisa lake; na si kuanzisha makundi yenye kubishana kwa kila moja kudai kuwa karibu sana na Mungu zaidi ya mengine. Kile alichokianzisha Mungu katika Samaria ni kuweka nguzo ya Kanisa lake lile lile; maana ***"walikuwa wafuasi wa makanisa ya Mungu yaliyo katika Uyahudi; katika Kristo Yesu…", soma 1 Wathesalonike 2:14.*** Kwa maana kwamba; baada ya kujiunga na Kristo, walishiriki nia moja iliyokuwa ndani ya Filipo, Petro na Yohana, wakawa wamoja pamoja na Baba na pamoja na Mwana, na baina yao wenyewe. Neno lililotumika hapa, **"makanisa",** kamwe halimaanishi makundi mengi yaliyo tofauti, bali linamaanisha kanisa moja katika maeneo mbali mbali. Na hii ndiyo maana tunaona kwamba; kama ni Petro au Paulo, ama kwamba ni Yakobo au mtumishi ye yote yule wa Mungu alipolitembelea kundi lo lote lile, kamwe hakuulizwa kwamba yeye anahusiana ama kushirikiana na akina nani *{yaani, ni wa kundi ama*

*kanisa gani},* ama kwamba yeye anaamini katika mafundisho gani. Kwa maana wote walikuwa katika mafundisho ya aina moja ya Kristo, ambaye alikuwa ndani yao wote na wao pia ndani yake.

Baada ya Petro kumtembelea Kornerio, Kanisa lilipanuka katika ukanda huo. Kundi lingine likatawanyikia upande wa Foinike na lingine Kipro na Antiokia; naam, hawa nao walikwenda wakilinena neno lile lile. ***"Mkono wa Bwana ukawa pamoja nao, watu wengi wakaamini, wakamwelekea Bwana. Habari hizo za watu hao zikafika masikioni mwa kanisa lililokuwa katika Yerusalemu; wakamtuma Barnaba, aende hata Antiokia", soma Matendo 11:19-22.***

Wapendwa; hapa pia tunaona kwamba; watu hawa hawakujitenga na kanisa mama, kwa sababu, tofauti na kupigania kuwa kama Kristo na kushuhudia ushuhuda ule ule po pote waendapo, hawakuwa na ajenda zao binafsi. Walifahamu ni jinsi gani Mungu anayatimiza makusudi yake kupitia kwao, ya kutaka kuufikia ulimwengu wote kwa Injili inayowakilishwa katika umoja na amani. Kwa hivyo, po pote walipokwenda walikuwa na kitu hiki kimoja katika nia zao. Kitu gani? ***"…kujitahidi kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani. Mwili mmoja, na Roho mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu. Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja. Mungu mmoja, naye ni Baba wa wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote" Waefeso 4:3-6.*** Na hili liliwezekana kutokana na kila mmoja kutothubutu ***"kutaja neno asilolitenda Kristo kwa kazi yake, Mataifa wapate kutii, kwa neno au kwa tendo" Warumi 15:18.*** Hatuoni mahali po pote katika biblia ambapo baadhi ya watu walijitenga na kuanzisha kitengo kingine cha huduma yao tofauti; kwa sababu baada ya kujikana nafsi, hakuna mtu mwenye kubakia na nia yake mwenyewe isipokuwa tu ya kutaka kuona na kusikia watu wakiupata ukweli wa Mungu kupitia kwake *{Agiza ujumbe wetu usemao,* ***"KUJIKANA NAFSI",*** *una maelezo zaidi kuhusu hili, na tutakutumia bure ili ujifunze zaidi}.* Na hii ni kwa sababu, kila mmoja alijitambua kuwa sehemu *{kiungo}* ya mwili wa Kristo, ambaye ni Kanisa. Hakuna aliyehitaji mwongozo wa namna ya kuzungumza *{ama kufundisha}* pindi walipoyatembelea makundi mengine katika maeneo mbali mbali yalikotawanyikia, maana wote walizungumza kitu kimoja ***{soma 2 Wakorintho 8:18-22,1-6}.*** Hata baada ya kutawanywa kwa mateso, Kanisa, ingawa ni kwa makundi ya ndani ya mikoa mbali mbali, liliendelea kuwa jamii moja japokuwa hakukuwa na kukusanyika wote katika sehemu moja. Washirika wake waliendelea katika nia ya Mungu ya umoja baina yao wenyewe.

Kila kundi lilihusika kuchangia ***"…kwa uwezo wao, na zaidi ya uwezo wao, kwa hiyari yao wenyewe walitoa vitu vyao; wakituomba sana pamoja na kutusihi kwa habari ya neema hii, na shirika hili la kuwahudumia watakatifu" 2 Wakorintho 8:3-4.*** Je! tuko hapo wapendwa? Haya ni makundi ya mataifa walioamini *{wa Makedonia ya Ugiriki/Uyunani},* ambao kwa upendo wa Mungu uliotenda kazi ndani yao, waliomba wapewe nafasi ya kutoa michango yao kuwasaidia watakatifu wengine. Je! ni Wamakedonia pekee ndio waliofanya hivyo? Wapendwa; Kanisa la Mungu lilisalia kuwa moja, na ndivyo lilivyo mpaka sasa. Kundi lingine lilianzishwa katika eneo la Antiokia ***{soma Matendo 11:20-22}.*** Na kundi hilo liliposikia

habari ya njaa iliyoikumba Yerusalemu na Uyahudi kwa ujumla; basi ***"…kila mtu kwa kadiri ya alivyofanikiwa, wakaazimu kupeleka msaada kwa ndugu zao waliokaa Uyahudi. Wakafanya hivyo, wakawapelekea wazee kwa mikono ya Barnaba na Sauli" Matendo 11:29-30.*** Kwa sababu ya nia moja ya Mungu kupitia kwa roho mmoja aliyekuwa ndani yao, ingawa walikuwa wametawanyika, lakini bado wote walikuwa ni Kanisa moja. Kutawanyika kwao kulikuwa ni kimaeneo *{yaani, umbali toka eneo moja walipo baadhi yao hadi eneo lingine walipo baadhi wengine},* na wala si tofauti ya maoni wala maamuzi yao.

Wapendwa; nafasi haitoshi ya sisi kuendelea na huu ufafanuzi, lakini yote yako katika Biblia *{**soma Warumi 16; 1 Wakorintho 16; Wafilipi 4;** pamoja na sura nyingine nyingi tu zinazoelezea jambo hili}.* Hatuoni hata sehemu moja katika Biblia ambapo Kanisa lilitofautiana katika kiwango cha kila kundi mahali lilipo kuanzisha huduma yake tofauti kwa kutoa udhuru na kukubali kutengana. Wakati Shetani alipojaribu kutaka kuligawa katika kipindi cha Mitume, wao kama mawakili wa kweli wa Mungu walisimama imara dhidi yake na kuikemea mipango hiyo, huku wakiuliza, ***"Je! Kristo amegawanyika? Je! Paulo alisulibiwa kwa ajili yenu? Au je! mlibatizwa kwa jina la Paulo?" 1 Wakorintho 1:13.*** Hapa Shetani alilivamia Kanisa kupitia kwa washirika wake wadogo *{yaani, wasio viongozi}.* Lakini kwa vile viongozi walikuwa watumishi wa kweli wa Mungu, ambao hawakuwa wabinafsi na walijawa na Roho Mtakatifu, waliliona jambo hili na mara moja wakalizuia.

Kwa hivyo, hawakushindwa kubuni njia ya kuwahamasisha washirika kukumbuka kile walichoamini na kile kilichoanzishwa ndani yao, ili kwamba ***"…nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja" 1 Wakorintho 1:10.*** Utawanyiko haukulizuia Kanisa kuwa moja katika mambo yote. Tofauti zilitokea baina ya mtu na mtu, lakini hawakuruhusu ziendelee kudumu. Waliendelea kuishi pamoja na umoja wao kuendelea. Soma habari za Paulo na Barnaba na Marko. Soma pia habari za wale wanawake wawili ***{Wafilipi 4:2}.*** Pointi yetu ni kwamba; pindi tofauti zilipoinuka, ilifanyika suluhisho na zikatupiliwa mbali tofauti hizo. Kwamba ni watu binafsi ama kundi katika Kristo, Kanisa lote liliendelea kuwa moja katika yeye, maana mfumo wake wa maisha ni ***"…kama inavyoipasa Injili ya Kristo,..kama mnavyosimama imara katika roho moja, kwa moyo mmoja mkiishindania imani ya Injili" Wafilipi 1:27.***

Naam; kwa sababu Injili inawafundisha watu wote kwa kuoneshwa na Kanisa kuhusu mfumo mmoja wa maisha ya umoja ya familia ya Mungu ambayo kila mmoja amekusudiwa *{ana nafasi}* kuyashiriki. Najua watu wengi, na hasa wenye kudhihaki, hivi sasa wanashangaa na kujiuliza ikiwa niko katika hali yangu ya kawaida kweli, na kama kweli nafahamu kile nisemacho! Hebu basi wale wanaodhania hivyo na wafahamu kwamba; si mimi, bali ni Bwana wenu Yesu Kristo, aliye kichwa cha Kanisa ndiye anenaye ndani yangu, na yeye ndiye kweli. Lakini mtu atajiuliza; "Liko wapi Kanisa hilo moja lenye umoja; maana kile tukionacho ni mamia ya makundi yajiitayo yenyewe kuwa ni **makanisa ya Mungu**, na kila moja likiwa na huduma yake yenye kujitegemea?" Basi eleweni na fahamuni kwamba; kila mshirika wa Kanisa la Mungu ametegemezwa katika Kristo *{ni kiungo cha mwili wa Kristo}.* Lakini katika Kristo

*{mwili mmoja},* kila mshirika ni mtegemezi kwa wengine, ili kwamba, ***"Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikamanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo" Waefeso 4:16.*** Sasa basi; ikiwa ndivyo ilivyo, je! unaweza kutuonesha mahali ambapo jambo hili linafanyika katika makundi ya leo? Hatuoni huu umoja *{mwili mmoja}.* Hebu twende pamoja tukaliangalie hili tafadhali.

## KANISA TOFAUTI

Paulo katika siku zake alitoa onyo kuhusu ***"ile siri ya kuasi"*** ambayo wakati huo ***"ilitenda kazi",*** *soma* ***2 Wathesalonike 2:7.*** Ni siri hiyo ndiyo itendayo kazi hivi sasa pia, na imefanikiwa kuyazaa makundi haya yote. Kwa sababu hiyo basi; jihadharini na manabii wa uongo, kadhalika pia na washirika wa kanisa wenye ufahamu mdogo wa Maandiko wanaojaribu kuhalalisha matengano ama migawanyiko. ***"Mlikuwa mkipiga mbio vizuri; ni nani aliyewazuia msiitii kweli? Kushawishi huku hakukutoka kwake yeye anayewaita ninyi. Chachu kidogo huchachua donge zima" Wagalatia 5:7-9.*** Mungu habadiliki kamwe, na anasema; ***"…shauri langu litasimama, nami nitatenda mapenzi yangu yote" Isaya 46:10.*** Kama tulivyoona mwanzoni; katika ulimwengu uliodanganyika na kugawanyikana; Mungu katika Kristo Yesu alilianzisha Kanisa lake ili kuonesha kusudi lake na maisha yake kwa wanadamu wote, ambayo ni ushirika wa umoja ukiwezeshwa kwa kushiriki nia yake moja. Tumelifuatilia Kanisa lake mpaka leo, na wala hatukuona mabadiliko yo yote yale. Sasa je! vipi kuhusu haya makundi? ***"Watoto, ni wakati wa mwisho; na kama vile mlivyosikia kwamba mpinga Kristo yuaja, hata sasa wapinga Kristo wengi wamekwisha kuwapo…" 1 Yohana 2:18.*** Tunajua kwamba haitasikika vizuri kwa walio wengi. Lakini wapendwa; je! itatusaidia nini tusipouongea ukweli wa Mungu ili tujifurahishe *{tujipendeze}* nafsi zetu wenyewe? *"Je! tuko hapa kutaka kuwapendeza wanadamu ama kumpendeza Mungu? Ikiwa mpaka sasa tunataka kuwapendeza wanadamu, basi sisi si watumwa wa Kristo",* ***soma Wagalatia 1:10.*** Je! kuna kuomba samahani *{kutaka radhi}* dhidi ya ukweli? La, hasha! Isipokuwa aliyejikwaa katika neno na atubu.

Mpinga Kristo ni mtu ye yote yule anayenena kinyume na Kristo. Na hiki ndicho kile ambacho haya makundi ya makanisa yanachofanya, na wanathibitisha kuwa ***"hao ni wa dunia; kwa hiyo wanena ya dunia na dunia huwasikia" 1 Yohana 4:5.*** Lakini watasema; *"Mnamaanisha nini? Mnayaita makanisa ya Mungu kuwa ni dunia?"* Tunasema, si makanisa ya Mungu. Na ndiyo maana yamebeba tabia ya asili ya ulimwengu ya matengano, huku pia yakinena kinyume na Kristo anayesema, ***"Wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu…" Yohana 17:21, soma pia 13:35*** *{agiza ujumbe wetu usemao,* ***"JE! KRISTO AMEGAWANYIKA?",*** *ili ujifunze zaidi, na tutakutumia bure ujumbe huo}.* Shetani aliyaanzisha makundi haya wakati alipowatuma mawakala wake ndani ya Kanisa la Mungu. Ni watu wanaojionesha kuwa kama malaika wa nuru *{kama waaminio}.* Inasikitisha kusema kwamba; Kanisa la Mungu la leo halionekani kujawa na

roho yule ambaye baba zetu waliotutangulia katika imani walionekana kuwa nayo. Kwa sababu katika kipindi chao, mbinu za Shetani zilipojipenyeza hata kidogo tu, Kanisa lilitambua na kutoa tahadhari; maana walionya wakisema, ***"…waangalieni wale wafanyao fitina na mambo ya kukwaza kinyume cha mafundisho mliojifunza; mkajiepushe nao. Kwa sababu walio hivyo hawamtumikii Bwana wetu Kristo, bali matumbo yao wenyewe; na kwa maneno laini na ya kujipendekeza waidanganya mioyo ya watu wanyofu" Warumi 16:17-18; soma pia 2 Petro 2:3-4.*** Kabla ya kufariki kwake; Paulo alionya kuhusu hili jambo linalofanyika hivi sasa, ambalo Shetani analifanya kupitia kwa mawakala wake. Sasa je! ni wangapi tunaoyakumbuka maonyo hayo na kujihadhari na hawa mbwa-mwitu? Hivi ndivyo ambavyo Shetani anayaanzisha makundi. Paulo alionya akisema; ***"Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu, alilolinunua kwa damu yake mwenyewe" Matendo 20:28.***

Kwa nini tahadhari? Kumbuka *{au tambua}* kwamba, Kristo anakushughulikia wewe unayeusoma ujumbe huu hivi sasa. Kile alichowaambia katika kipindi kile ambacho mambo haya yaliandikwa, ndicho kile anachotuambia sisi tunaosoma sasa, maana yeye habadiliki kamwe. Je! utakumbuka? Sasa basi; kwa nini tahadhari? Paulo anaongeza kusema; ***"…mbwa-mwitu wakali*** *{mawakala wa Shetani}* ***wataingia kwenu, wasilihurumie kundi; tena katika ninyi wenyewe watainuka watu wakisema mapotovu, wawavute hao wanafunzi wawaandamie wao" Matendo 20:29-30.*** Je! tuliyakumbuka maonyo na kuchukua tahadhari? Kamwe hatukufanya hivyo hapo kabla; maana makanisa haya tunayoyashuhudia leo hii ni matunda ya kazi ya Shetani. Lakini watu wa Mungu wa kweli wamezamishwa kiasi cha kutoweza kuona, na wengi wao wamegharikishwa na kusombwa na mfumo huo. Unasema, *"Mimi ni wa United, ama wa Living, ama wa Restored, ama wa Church of God in truth, ama wa kundi {kanisa} lo lote lile"*. Katika kipindi cha Mitume, Shetani alijaribu kuwatumia waumini katika kusababisha migawanyiko kwa kuwafanya kila mmoja wao kushikana na mitume kwa namna ya upendeleo ama ubaguzi ***{tafadhali soma 1 Wakorintho 1:11-12}.*** Basi watumishi wa kweli wa Mungu wakaliona hilo na kupaza sauti ya kugutusha *{ya tahadhari}*. Leo hii, Shetani anawatumia viongozi, na wafuasi wanyofu wamekuwa wajinga. Mpendwa; usihisi *{ama usidhani}* kwamba unatukanwa ama kubughudhiwa Kristo anapokuambia kuwa hivi sasa uko katika utumwa wa kiroho. Tafadhali litazame jambo hili kwa nia yenye kujikana nafsi. Shetani amewainua watumishi wake *{mbwa-mwitu}* katika kanisa. Wamewagawana wafuasi na kila mmoja akitafuta kufuatwa yeye na si kuwasilisha ujumbe wa Mungu ***{soma Matendo 20:30}.***

Sasa basi; ikiwa wao ni mbwa-mwitu; je! kile wanachokileta kwa jina la kanisa ni cha Mungu? La, hasha! Wale ambao mlituuliza kuhusu mahali ambapo kanisa limefafanulikwa na maandiko kuwa ni kanisa la mwili mmoja, pateni majibu yenu basi katika pointi hii tafadhalini. Soma kwa makini na upate jibu ulilolitafuta *{unaweza pia kuusoma ujumbe wetu usemao,* ***"KANISA LA SIKU ZA MWISHO",*** *kwa msaada zaidi}*. Hawa mawakala wamewekwa na Shetani na wanatimiza unabii wa kuja kwa uasi kutoka katika msingi wa kweli ***{soma 2 Wathesalonike 2:3}.*** Katika kipindi cha karne ya kwanza, Kanisa lilitawanywa kwa mateso.

Utawanyiko wa leo unasababishwa na udanganyifu, kwa watu kuukubali uongo, na kila mmoja kuwafuata mawakala ambao wanafundisha yale wayatakayo kuyasiki *{wayapendayo}*, na wamegeuka na kuiacha kweli ***{soma 2 Timotheo 4:3-4}.*** Wengi wa hawa viongozi ni watu ***"…wenye kudhihaki, wakizifuata tama zao wenyewe za upotevu*** *{kutafuta wafuasi}.* ***Watu hao ndio waletao matengano, watu wa dunia hii tu*** *{si wa Mungu kama ambavyo wengine wanadai kuwa},* ***wasio na Roho" Yuda 1 :18-19.***

Mtumishi wa Mungu alilionya Kanisa kuhusu mawakala wa Shetani walio ndani. Alipokuwa akiwaonya washirika, alizungumza na kundi la watu wapatao mia mbili hivi, na aliwaambia; *"Nina mashaka kwamba huenda katika kusanyiko hili kama kuna watu zaidi ya watano au angalahu kumi wanaoupata ukweli huu ipasavyo"*. Tunachokisema na kumaanisha hapa ni kwamba; katika kila kusanyiko la Kanisa la Mungu, walio wengi ndani yake ni mawakala wa Shetani! Na hii ni kwa sababu, kama Kristo alivyosema; ni wachache sana wanaoiona na kutembea katika njia nyembamba. Na japokuwa ni wengi walioitwa, lakini wateule ni wachache sana! Shetani anawatumia hawa mawakala kuwararua hawa wachache wanaotaka kukutana katika mwamvuli wa ushirika wa kiroho. Na kwa sababu hawakuchukua tahadhari, basi pindi Shetani alipowapiga, walichukuliwa mbali na hawa mbwa-mwitu walio wengi ambao ni walaghai. Kwa hivyo, elewa na fahamu kwamba, Kanisa moja la kweli la Mungu bado liko hai, lakini limetapanywa na nguvu za Shetani kupitia kwa mawakala wake wanaoonekana hivi sasa kama viongozi wa makanisa; na wamewawekea uzio. Kwa madai ya kulilinda kundi, wamewafanya kuamini kwamba wanaweza kuabudu na kuwa huru tu na wale wanaoshiriki nao katika kundi lao. Je! tunamshambulia mtu ama kundi fulani au hii ndiyo hali halisi iliyopo? Utakubaliana nasi kwamba, kila kundi linajiona kuwa ndilo zuri na la hakika miongoni mwa makundi mengine. Ugeni wo wote ule wa mshirika wa kundi lingine kwenda katika kundi tofauti hupokelewa kwa tuhuma kubwa, pasipo kujali kwamba huenda mtu huyo amekuja na ukweli. Wanachojali ni ikiwa mtu huyo amekuja kuungana nao. Na endapo hakuja kuungana nao; basi kile kifuatacho ni hoja za kuwaambia washirika kujihadhari na mtu huyo!

## WATAMBUE KWA MATUNDA YAO

Ulimwengu huu ni ulimwengu wa Kishetani. Baada ya watu kuikubali njia yake; wameishi kwa matengano, masengenyo, kujiwekea mipaka, kupenda ukuu *{kujikweza}*, na mengine mengi kama haya. Kadiri tunavyoendelea kulifikia Kanisa katika Ulaodikia ndani ya makundi haya; viongozi wengi wa makanisa wanatulaumu na kutushutumu kwamba tunawavamia waumini wao. Baadhi yao wanauliza; *"ni kwa nini tunawahubiri washirika wao badala ya kwenda kuhubiri kule {wanakokuita} ulimwenguni?"* Eti, Ulimwenguni! Je! hawafahamu kwamba wao wenyewe tayari wamo ulimwenguni, na ndiyo maana wanajali sana nafasi za uongozi wao kiasi cha kuyatupilia mbali yale ayasemayo Kristo wanayedai kwamba wanamtumikia? Wanadhani tuko kama wao, na hivyo kwamba tumekuja kuwapindua na kuwavuta wafuasi wao watufuate sisi. Je! sisi tuliopewa kazi ya kulichunga kundi tunalichunga

kwa kuwajengea kuta kuwazunguka? Je! hatufahamu kwamba Shetani hutenda kazi katika mioyo *{nia/akili}* ya watu na hawezi kuzuilika kimwili? Kanisa la kweli la Mungu kamwe halipiganii kupata wafuasi. Na badala yake; linalitimiza agizo la Bwana wake la kuwaonya washirika wake ambao hivi sasa wametapanywa katika haya makundi *{makanisa}* kwamba, ***"Kimbieni kutoka kati ya Babeli*** *{machafuko ya kiroho},* ***kila mtu na ajiokoe nafsi yake".*** Kwa nini? Kwani kitu gani kinafanyika? ***"Bwana asema hivi, Angalia, nitaamsha juu ya Babeli…upepo uharibuo" Yeremia 51:6,1.***

Lakini vile vile; Kanisa la kweli halijipiganii lenyewe, bali linaipigania kweli, na kulilinda kundi lake kwa ***"…kuwakamilisha watakatifu*** *{kwa ufahamu wa maandiko},* ***hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe; hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo; ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu" Waefeso 4:12-14.*** Lakini kinyume na ukweli huu ulio wazi; hawa viongozi hawawezi kuruhusu asiye mmoja au mshirika wao kufundisha katika masinagogi yao pasipokujali kwamba mtu huyo anafundisha ukweli ambao ye yote mwenye nia ya kutenda mapenzi ya Mungu atauthibitisha mwenyewe kwa maandiko na si kutoka kwa mhubiri huyo. Ni katika namna ile ile ambayo viongozi wa dunia wanaitumia katika kulinda masilahi yao na kutoruhusu wengine kuinuka juu yao, ndivyo ambavyo hawa viongozi wa makanisa nao wanavyofanya. Wana ubaguzi, ni wenye kuwaheshimu matajiri na viongozi wa nyadhifa mbali mbali za juu katika jamii, naam; wanafanya vile vile kama ulimwengu ufanyavyo.

Tunafahamu kwamba hivi sasa Mungu anajenga fikira, nia, hisia, ufahamu, na tabia yake ndani ya mioyo ya waaminio. Kwa hivyo Kanisa la kweli linajali hayo pamoja na ushirika uhusuo neno la Mungu linaloizungumzia mioyo yao na kuwaonesha yale wapaswayo kuyafanyia mabadiliko. Bali ushirika wa makundi haya umejawa na kutazama viwango baina yao wenyewe. Wanathathmini maisha ya watu vile vile kama ulimwengu ufanyavyo. Kwa nini? Kwa sababu baada ya kuupoteza ukweli, malengo yao yamegeukia katika viwango vya kimwili ambako wanafikiria tu mambo ya mwili ***{soma Warumi 8:5}.*** Ni hayo tu ndiyo wayafahamuyo. Wanajibidiisha katika ***"kujipima nafsi zao na nafsi zao, na kujilinganisha nafsi zao na nafsi zao*** *{si kujilinganisha na Kristo},* ***hawana akili", soma 2 Wakorintho 10:12.*** Naam; wanajiepusha mbali na mjadala wo wote ule unaozigusa mioyo yao, kwa sababu nia zao hivi sasa si kuwa sawa na Kristo, bali ni kulinda misimamo *{itikadi}* yao. Wanachojali ni kuhusu jinsi gani watu wengine *{si Mungu}* wanavyowatazama; wanasema nini juu yao; wanawachukuliaje; wanazitazamaje nafasi zao za uongozi na mengine mengi kama haya; kwa sababu mkiwa katika viwango vya kimwili, ***"Mwawezaje kuamini ninyi mnaopokeana utukufu ninyi kwa ninyi, na utukufu ule utokao kwa Mungu aliye wa pekee hamwutafuti?" Yohana 5:44.*** Ukiwa pale miongoni mwao, na ikiwa unaongozwa na roho mtakatifu na kupigania kuwa kama Kristo; basi utakubaliana nasi kwamba, kile unachokipata pale ni vikwazo tu, maana walio wengi kwa maneno na matendo yao wanajaribu kukutoa katika kumfikiria Mungu. Je! wewe ni miongoni

mwa wale wanaoyashuhudia hayo pale ulipo? Ikiwa ndivyo; basi hii ni kwa sababu uko katika Babeli ya kiroho na umebanwa hapo, huku ukidhani ya kuwa wale wanaokuzunguka *{washirika wenzako}* wana mwelekeo ulio kama wako, na kwa wakati huo huo ukijiuliza na kushangaa, ni kwa nini hawako makini *{hawayachukulii kwa uzito}* na maisha ya Mungu? Basi elewa na fahamu kwamba uko katika mazingira ya Kilaodikia. Mshukuru sana Mungu kwa sababu hii sauti unayoisikia kwa kusoma ujumbe huu, ni sauti ya Mwokozi wako kupitia kwa wale walioisikia kabla yako; na ambao sasa Kristo anawatumia kukuita kutoka hapo ulipo ili umrudie yeye *{na sio sisi; japokuwa ukimrudia yeye, utaunganishwa nasi pia, maana tunaongea ndani yake},* maana, ***"hatuthubutu kutaja neno asilolitenda Kristo kwa kazi yetu, Mataifa wapate kutii, kwa neno au kwa tendo", soma Warumi 15:18.***

Wapendwa; ikiwa tu miongoni mwa wale walionaswa mahali; basi isikilize hii tarumbeta na kuikumbuka, kwa sababu ni agizo la Kristo la kulikusanya Kanisa lake na kuliandaa kwa ***"kulitakasa na kulisafisha kwa maji katika neno {Waefeso 5:26}",*** na hii ni kwa sababu ujio wake wa mara ya pili umekaribia sana. Sasa basi wapendwa; kwa vile tunatarajia kuurithi ufalme ule ujao hivi punde, na huku hili likiwezekana tu ikiwa Kristo anakaa ndani yetu na sisi pia ndani yake *{yaani, katika neno lake};* basi yuko hapa hivi sasa akikuambia kwamba, umemtelekeza; bali yeye hajakata tamaa na wewe. Alikuja ndani yako pindi ulipoamini na kufanya makao ndani yako, na kukufanya kuwa umoja pamoja naye na pamoja na Baba, na pamoja na wale waaminio kama wewe. Lakini mara baada ya uvamizi wa mbwa-mwitu, umechukuliwa mbali naye. Na kwa hivyo, anahitaji umrudie tena; na hii hapa ni ahadi yake kwako kwamba; ***"Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake*** *{kama alivyokuwamo mwanzoni},* ***nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami" Ufunuo 3:20.*** Mara tutakapofanya hivyo na kuwa wakamilifu kwa kulitii neno, kwa uwezo wa Mungu hatutakuwa na mawaa. Kwa hivyo Kristo anaendelea na ahadi yake kwako wewe uisikiaye sauti hii akisema; ***"Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi, kama mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake" Ufunuo 3:21.*** Wale wote watakaotoka katika Ulaodikia wataketi pamoja *{si kwa makundi yenye kutofautiana}* katika kiti cha enzi cha Kristo. Mungu anahitaji Kanisa lake lijifunze katika umoja huo hivi sasa na kwamba lipate kukua katika tabia hii ya umoja. Ikiwa tunahitaji kuwepo pale, ni lazima tuyashinde haya matengano na migawanyiko hii hivi sasa. Ikiwa tunahitaji kuketi pamoja naye katika kiti chake cha enzi, basi ni lazima tujifunze kuishi pamoja hivi sasa; maana, ***"po pote ulipo mzoga*** *{Kristo},* ***ndipo watakapokusanyika tai*** *{Kanisa lake la kweli}****" Mathayo 24:28.*** Na kwa sababu hiyo basi wapendwa; ***"Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa" Ufunuo 3:22.***

Kristo yuko hapa, amesheheni mambo mengi ambayo yuko tayari kuwafundisha wale wanaotamani kuyafahamu maisha yake ya uzima wa milele katika ufalme wake ujao hivi punde hapa duniani; naam, kupitia kwa Kanisa lake, anaziweka wazi habari hizo. Basi tafadhali msikilize yeye kupitia kwetu sisi watumwa wake aliotutuma kwako.

Tunayo majarida pamoja na vitabuvingi vyenye mada *{masomo}* mbali mbali za Biblia. Huduma yetu inatolewa bure kabisa kwako bila malipo yo yote utakayotozwa, maana Kristo ametuagiza akisema, ***"…mmepata bure, toeni bure. Msichukue dhahabu, wala fedha, wala mapesa mishipini*** *{ama mifukoni}* ***mwenu" Mathayo 10:8-9.*** Kwa hiyo wewe kazi yako ni kuagiza tu kile/vile utakavyohitaji, nasi tutakutumia bure huko uliko kwa gharama zetu.

Baadhi ya majarida yetu ni kama vile; WAPI PA KUANZIA?, THAMANI YA UKRISTO, HUYU NI SHETANI, MITI MIWILI, SHERIA ZA KIAFYA, KUOKOLEWA KWA NEEMA, SHETANI NI NANI?, ROHO YA SABATO ZA BWANA, JE! WEWE NI MKRISTO?, KWA NINI SHERIA? MNYAMA WA UFUNUO, n.k.

Pia baadhi ya vitabu vyetu ni kama vile; UFALME WA MBINGUNI, KIFO NA KIYAMA, SIKUKUU ZA MUNGU, AMRI KUMI, KUFA NA KUFUFUKA KWA YESU, DINI ZA MITINDO, n.k.

Waweza pia kuuliza swali/maswali yahusuyo mafundisho ya Biblia, nasi tutakutumia jarida ama kitabu chenye majibu sahihi ya maswali yako. Ifahamike kwamba; mafundisho yetu hayaegemei dhehebu lo lote lile la kidini, bali tunafundisha ukweli halisi wa Biblia kwa watu wa imani zote. Kwa hivyo kama unahitaji kuyafahamu maandiko katika uhalisia wake; basi wasiliana nasi kwa anuani zifuatazo:-

**KANISA LA MUNGU – TANZANIA**

**Idara ya uchapaji na usambazaji: MWANZA**

**Simu: +255 753 359 179, +255 688 359 179 na +255 655 659 179**.

**Barua pepe: Ukweliwabiblia@yahoo.com.sg**

**Idara ya usambazaji:**

**RORYA – MARA, - Simu: +255 755 409 202.**

**ARUSHA, - Simu: +255 754 028 574 na +255 782 422 216.**

**DAR ES SALAAM, - Simu: +255 762 055 056 na +255 672 611 204.**

**KENYA, - Barua pepe: endcog@gmail.com**

***Neema na rehema za Bwana wetu Yesu Kristo na ziwe pamoja nanyi. Utukufu na uweza una yeye tangu milele, sasa na hata milele. Amina.***